

Maelezo ya Utunzaji

Kunyonya kwa Mtoto Akiwa Macho/Akiwa Amelala

	Niko tayari kula	Sili vizuri
Kabla ya Kunyonya	Anaamka mwenyewe kila masaa 2-3	Haamki mwenyewe ili kula kila masaa 3
Kunyonya	Kunyonya Vizuri: <ul style="list-style-type: none"> Anashikilia matiti kwa angalau dakika 10 Kunyonya kwa mtindo wa kunyonya mara 8-10 au zaidi kisha kumeza Anaweza kusitisha kwa sekunde 5-10 Anaweza kutumia mkono kufinya matiti Unaweza kufanyia mtoto masaji ili kumsisimua 	Kunyonya kwa Njia Isiyo Nzuri: <ul style="list-style-type: none"> Ananyonya akiachilia Ananyonya kwa chini ya dakika 10 Anasita kwa Vipindi Virefu Haitikii kulisimuliwa au kufinywa kwa matiti kwa kunyonya vizuri zaidi
Je, Anafungua Taya kwa Upana?	Ndiyo	Hapana
Je, Anameza maziwa kwa sauti?	Ndiyo	Hapana
Je, Kuna Uchungu kwa Chuchu	Hapana	Ndiyo
Maelekezo	Ikiwa dalili hizi zipo, endelea na kipindi cha kunyonyesha kwa hadi dakika 20 kwenye titi la kwanza, kisha umteue na umnyonyeshe titi la pili.	Ikiwa dalili hizi zipo, acha kunyonyesha, kamua maziwa, na umlishe maziwa ya mama/fomula kwa chupa. Jaribu kumnyonyesha katika kipindi kinachofuata
Baada ya Kumlisha	<ul style="list-style-type: none"> Chuchu ni ndefu na ya mviringo Mtoto ana furaha Matiti ni laini Kiasi cha maziwa kwenye pampu ya matiti ni kidogo baada ya kunyonyesha 	<ul style="list-style-type: none"> Chuchu imepinda au imekunjwa Mtoto analialia Matiti yanabakia yakiwa yamejaa maziwa Kiasi cha maziwa kwenye pampu ya matiti hubaki sawa na bila kunyonyesha
Kila siku	<ul style="list-style-type: none"> Angalau nepi 6-8 zilizojaa mkojo kabisa Angalau nepi 3 za kinyesi za rangi ya manjano 	<ul style="list-style-type: none"> Chini ya nepi 6-8 zilizojaa mkojo Chini ya nepi 3 za kinyesi cha rangi ya manjano Piga simu kwa daktari wa mtoto wako Lisha mtoto kwa chupa na kunyonyesha

- Uliza mshauri wako wa kunyonyesha akusaidie kunyonyesha ukiwa hospitalini. Wanaweza kukusaidia kwa njia za kumwamsha mtoto wako, kumsaidia mtoto kushika matiti, na kutumia pampu ya kukama maziwa.

10/2023

Maelezo haya hayachukui nafasi ya ushauri wa mtoa huduma wako wa matibabu, mpango wa tiba, au elimu inayotolewa na muuguzi au mtoa huduma wako mwingine. Hakikisha unafuata mpango wako kibinafsi wa huduma. Hakuna chochote kwenye laha hizi kinachochukuliwa kuwa ushauri wa kimatibabu, utambuzi au matibabu. Ikiwa una maswali kuhusu maelezo haya au mengine yoyote ya kimatibabu, zungumza na mtoa huduma wako. Omba usaidizi moja kwa moja ikiwa unahitaji huduma za matibabu za dharura. Ikiwa uko nje ya hospitali, piga simu kwa 911. Ikiwa wewe ni mgonjwa uliye hospitalini, omba usaidizi kutoka kwa muuguzi wako au mhudumu mwingine yeyote wa timu yako ya huduma.

Muulize mfanyakazi kuhusu wakalimani na huduma na vifaa vingine vya ufikiaji wa lugha, vinavyopatikana bila malipo kwa wagonjwa na familia. Pregúntenos acerca de los intérpretes y otros servicios y ayuda para el acceso al idioma que están a su disponibilidad sin costo alguno.

